**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule 0743444922**

**Makamu Mkuu wa Shule 0744080070/0755485388**

**Matron/Patron 0766644555**

**SHULE YA SEKONDARI MAKAMBAKO**

**S.L.P 1120 MAKAMBAKO**

**Tarehe ....................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAKAMBAKO HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO MKOA NJOMBE MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Makambako ipo umbali wa Kilometa 1 Kaskazini/Kusini/Mashariki/Magharibi mwa Mji wa Makambako Usafiri wa tax na bajaji kutoka stendi unapatikana Nauli ni Shilingi 500 kwa bajaji na tax ni shilingi 2,000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/08/2023

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sweta rangi ya blue yenye shingo V (2)
ii. Suruali rangi ya Damu ya mzee ISIYOBANA (kitambaa cha Istimu 1) (2)
iii. Gauni jeupe fupi lenye marinda (2) picha imeambatanishwa
iv. Tai fupi 2 rangi ya suruali
v. Viatu vyeusi vya kufunga na Kamba vyenye kisigino kifupi pea (2)
vi. Soksi Nyeusi jozi mbili
vii. Tshirt za Blue 2
viii. Sare ya michezo – tracksuit rangi ya blue Bahari
ix. Nguo za kushindia ( shamba Dress) kitambaa aina ya satini Rangi darkblue -mshono solo solo Dress mbili (2)
x. Rangi ya Hijab (kijuba) ni Nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (*naambatanisha mshono*);

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro 2 $^{1}/_{2}$ x 12
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink , blanket 1, chandarua 1
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hizo ziwekwe katika akaunti ya namba 60310017593 na mwanfunzi aje na pay in slip original na sio copy**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- **Mwanafunzi apewe fedha ya kujikimu ya kutosha kuepusha usumbufu,tunashauri afunguliwe Akaunti NMB,CRDB,NBC NA POSTAL BANK ambazo zipo Makambako.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;

xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA**

**SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- ➢ **Mkuu wa shule 0743444922**
- ➢ **Makamu Mkuu wa Shule 0744080070/0755485388**
- ➢ **Mwandamizi Taaluma 0765264350**
- ➢ **Mwandamizi Malezi 0757001983/0768102971**

## i. TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi……………………………………
2. Mahali alipozaliwa Wilaya……………………………….Mkoa…………….
3. Tarehe ya Kuzaliwa…………………………………………………………
4. Dini………………………………Dhehebu…………………………………..
5. Shule aliyotoka……………………………………………………………..
6. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama vile Mpira wa Miguu,Mpira wa Mikono, Mpira wa Pete n.k ……………………………………………………

Sahihi ya Mwanafunzi……………………Tarehe…………………………………

## ii. HABARI ZA WAZAZI

1. Baba yu hai? Ndiyo / Hapana. Jina la Baba…………………………………….
2. Mama yu hai? Ndiyo/Hapana Jina la Mama……………………………………
3. Jina la Mzazi/Mlezi anayekulea (kama 1 au 2 hapo juu ni Hapana)…………….
4. Na ya Simu ya mlezi/mzazi……………………………………..
5. Uhusiano wako na Mlezi…………………………………………
6. Kazi ya Mzazi/Mlezi……………………………………………….
7. Anwani ya Mzazi/Mlezi……………………………………………
8. Mahali ambapo Mzazi/Mlezi anaishi
   Kijiji/Mji……………………………Kata…………………………Tarafa………………
   Wilaya……………….Mkoa……………. Na. ya Simu……………………..
   Sahihi ya Mzazi/Mlezi………………………………………Tarehe………………

## iii. NDUGU WENGINE WA KARIBU

| JINA | UHUSIANO | ANUANI YAKE | SIMU |
|---|---|---|---|
| 1……………………….. | …………………… | ………………… | ………………. |
| 2……………………….. | …………………… | ………………… | …………….. |
| 3 ………………………. | …………………… | ………………… | …………….. |

### iv. SHERIA ZA SHULE

- **HESHIMA**

Wanafunzi wanatakiwa kuwaheshimu walimu, Wafanyakazi Wasio Walimu na Wanafunzi wenzake pamoja na watu wengine walioko ndani na nje ya shule. Wanafunzi hawa ruhusiwi mambo yafuatayo:-

- **MAHUDHURIO**

Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria "Assembly" Ground Asubuhi kabla ya masomo kuanza na mchana baada ya masomo kumalizika. Pia wanatakiwa kuhudhuria darasani kulingana na taratibu za vipindi na kwenye Mikutano yote halali itakayo itishwa na uongozi wa Shule.

- **MAANDALIO YA JIONI**

Wanafunzi wote wanatakiwa kujisomea kuanzia saa moja hadi saa Nne usiku kila siku bila kukosa.

- **KUWAHI**

Wanafunzi wanatakiwa kuwahi asubuhi (saa 1.00 kamili) siku za masomo, na wanaporudi kutoka likizo wanatakiwa kufika saa 11.00 jioni. Atakayechelewa atatakiwa kuja na Mzazi/Mlezi kuthibitisha sababu za kuchelewa kwake.

- **SARE YA SHULE**

  Wanafunzi wanatakiwa wavae Sare zinazokubalika na Shule. Wakati wa masomo Darasani, wanapokwenda makwao kwa ajili ya likizo na wanaporudi Shule baada ya likizo.

- **MIPAKA YA SHULE**

Wanafunzi hawatakiwa kutoka nje ya Mipaka ya Shule bila kibali maalumu. Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia nyumba za Walimu, Watumishi Wasio Walimu na Ofisi za shule bila ruhusa..

- **USAFI**

Wanafunzi wanatakiwa wafanye usafi wa mwili, Mazingira ya nje, Madarasa yao na Bwenini.

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**

Makambako Secondary School,
P. O. BOX 1120
MAKAMBAKO.
Date………………

The Medical Officer,
………………………
………………………
………………………

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please kindly, examine (Name)……………………………………………To Determine her Physical and Mental fitness for pursuing Secondary School Studies.

FWILLA, G.H.
HEADMASTER

1. Eyesight…………………………………………………………………
2. Hearing…………………………………………………………………
3. Spleen…………………………………………………………………...
4. Limbs…………………………………………………………………
5. Leprosy…………………………………………………………………
6. Epilepsy…………………………………………………………………
7. Cardiac diseases………………………………………………………
8. Rheumatism……………………………………………………………..
9. Venereal diseases……………………………………………………..
10. Pregnancy………………………………………………………………
11. Any other serious diseases……………………………………………
    ………………………………………………………………………………
12. General coments………………………………………………………
    ………………………………………………………………………………

Name………………………………………………
Signature…………………………………………
Stamp………………………………………………..

**ORODHA YA VITABU**

Nunua Vitabu vya masomo uliyochaguliwa kuja kuyasoma kama kama inavyoonesha hapa chini:-

| **NA.** | **VITABU VYA KIADA** | **VITABU VYA REJEA** |
|---|---|---|
| | BIOLOGY 1 | 1.Biological Science by Taylor |
| 1 | TIE – Biology For S. S.<br>Form V | 2. Biology class XI 4 11 Boys. Chanels. |
| 2 | TIE – Biology for S.S. Form VI | 3.New understanding Biology for Advance level by Glenn and susain. |
| | | 4.Guide to Dissection By Ranett |

| | | |
|---|---|---|
| | **CHEMISTRY** | |
| 1 | CHEMISTRY FOR SEC.S CHOOL FORM V<br>TIE. | CON CEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XI VEL 1 7 II BY S. CHANO. |
| 2 | CHEMISTRY FOR SEC.SCHOOL FORM VI<br>TIE | CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XII VOL.I & VV BY S. CHANO |
| 3 | ADVANCED LEVEL IN ORGANIC CHEMISTRY TIE (PART A and B. | ORGANIC CHEMISTRYY PART A and B BY<br>CHEMSTRY PART A & B BY M.TR M. H. NKUNYA (MZUMBE BOOK PROJECT) |
| 4 | ADVANCED LEVEL INORGANI CHEMISTRY TIE PART B | UNDER RSTANDINGG CHEMISTRY. |

**ORODHA YA VITABU VYA KISWAHILI KIDATO CHA TANO NA SITA.**

1. SARUFI MAUMBO YA KISWAHILI SANIFU (SAMAKISA) SEKONDARI NA VYUO

   Mwandishi Y. M. KIHORE.

   D.P.B MASSAMBA

   Y.P. MASANJILA
2. SARUFI MIUNDO YA KISWAHILI SANIFU (SAMIKISA) SEKONDARI NA VYUO
3. NADHARIA YA LUGHA MASEBO & NYANGWINE
4. ISIMU NA LUGHA. MGULLU R.
5. FASIHI KIDATO CHA TANO MASEBO & NYANGWINE.
6. TAHAKIKI YA FASIHI KIDATO CHA TANO NA SITA: MUSSA SULEIMAN.

**1. ADVANCE MATHEMATICS.**

(a) Advanced Mathematics, for A-level By tie.

(b) Pure Mathematics 1 and 2 By Bank House.

(c) Core course Advanced Mathematics. By Bostch and chandler.

(d) A coucuse course in Advanced level Stalistics By Crawshal and J. chamber.

**2. BASIC APPLIED MATHEMATICS.**

(a) Basic Applied Mathematcs By tie.

(b) Pure Mathematics 1 and 2 By Bank HOUSE

(c) Core course mathematics By Bostoch and chandler.

**GEOGRAPHY A – LEVEL**

1. General Geography In Diagrams (R>B> Bunnett)
2. PRINCIPLE OF PHYSICAL GEOGRAPHY F.J. MONK HOUSE.
3. PLACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA BY PRICHARD. 4. LAND FORMS FOR AFRICA COLLIN BAKOR

**HISTORY I & II.**

(1) Kato A Kassim (2012) - Mastering Advanced Level History Paper I & II.By Move as Book Publishers and Suppliers Mwanza.

(2) Tumaini George (2010) Understanding African History paper I & II motes ED. By Mr Antony E. Fungilayo.

(3) SHIBITALI C.K. TUMAINI (2013) - Contemporary History cal events Advanced
Level History 2 and History, Published by shibitali
and Sons Publishees, Dar es Salaam Tanzania.

(4) Poncizn I & Mpambile C.J. (2009) - Focus on world. History Advanced level History sysllabus. History 1 and 2, Prited type
set AND Published by Nile Publisher Dar es Salaam`
Tanzania.

**ACCOUNTANCY BOOKS**

(1) S. KAMTANDE – Advanced Accountancy (2016)

(2) S.N MAHESHWARI- Advance accountancy (vol 1 & II

(3) Frank wood business Accounting (11th edition) (Accounting I & II)

(4) REVIEW BOOKS (I & II) BY APE

(5) N.A SALEEMI, SIMPLIFIED Accounting (I & II)

## MFANO WA SARE YA SHULE KWA WANAFUNZI WASICHANA

